JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001 : 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



MACHI 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

MACHI 2025

# YALIYOMO

**NENO LA MWENYEKITI WA BODI ..... iii**
**DIBAJI ..... iv**
**VIFUPISHO VYA MANENO ..... v**
**VIPIMO NA ALAMA ..... v**
**FASILI YA VIASHIRIA VIKUU VYA UTENDAJI ..... vi**
**UTENDAJI KAZI WA MAMLAKA ZA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA ..... viii**

**SURA YA KWANZA ..... 1**
**1.0 UTANGULIZI ..... 1**
1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji ..... 2
1.2 Dira na Dhamira ya EWURA ..... 2
1.3 Lengo la Taarifa ..... 2
1.4 Mchanganuo wa Mamlaka za Maji ..... 3
1.5 Nyenzo za Uandaaji wa Taarifa ..... 5

**SURA YA PILI ..... 6**
**2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTENDAJI ..... 6**
2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji ..... 6
2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji ..... 7
2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji ..... 8
2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira ..... 9
2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka ..... 9
2.6 Upotevu wa Maji ..... 10
2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji ..... 11
2.8 Utendaji wa Kifedha ..... 13
2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja ..... 15
2.10 Huduma kwa Wateja ..... 15
2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa ..... 16
2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita ..... 16
2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji ..... 17
2.14 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi ..... 18
2.15 Hali ya Taasisi ..... 18

**SURA YA TATU ..... 19**
**3.0 USHINDANISHAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI ..... 19**
3.1 Taratibu za ushindanishaji ..... 19
3.2 Matokeo ya Ushindanishaji ..... 19

**SURA YA NNE ..... 25**
**4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO ..... 25**

**SURA YA TANO ..... 29**
**5.0 HITIMISHO ..... 29**

## NENO LA MWENYEKITI WA BODI

Ninayo heshima kuwasilisha Muhtasari wa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mamlaka za Maji) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Taarifa hii ni ushuhuda wa dhamira yetu ya kuhakikisha Mamlaka za Maji zinatoa huduma za maji na usafi wa mazingira zilizo salama, za kuaminika, na endelevu.

Huduma za maji na usafi wa mazingira ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya binadamu. Kutambua umuhimu wake, Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 zinasisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma hizi. Miongoni mwa vipaumbele vya nyaraka hizi za kimkakati ni pamoja na kuboresha miundombinu ili kuwezesha ufanisi na huduma endelevu za maji na usafi wa mazingira.

EWURA imepewa jukumu chini ya Sheria ya EWURA, Sura ya 414, na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272, kusimamia huduma za maji na usafi wa mazingira zinazotolewa na mamlaka za maji. Katika kutekeleza jukumu hili, EWURA inahakikisha kuwa mamlaka hizi zinatoa huduma bora za maji na usafi wa mazingira kwa kuzingatia ufanisi, utendaji bora wa kiuchumi na ubora wa huduma kwa kuzingatia malengo yaliyoainishwa kwenye nyaraka za kimkakati za kitaifa.

Katika kipindi cha taarifa hii, EWURA imepiga hatua katika kuhakikisha kuwa mamlaka za maji zinatimiza malengo ya kimkakati ya kitaifa katika utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Mafanikio yaliyoainishwa katika taarifa hii ni matokeo ya juhudi zetu za pamoja za kuboresha ufanisi wa kiutendaji, kupanua wigo na kuboresha huduma licha ya changamoto zilizopo.

Lengo letu ni kuendelea kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira ambazo ni endelevu, jumuishi na himilivu. Niwahakikishie dhamira yetu ya kuhakikisha utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini inabaki kuwa msingi wa maendeleo ya taifa.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa Wizara ya Maji, Wizara ya Afya, Mamlaka za Maji, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), na wadau wote wa sekta ya maji na usafi wa mazingira kwa michango na ushiriki wao katika maandalizi ya taarifa hii. Pia, naishukuru Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, menejimenti na wafanyakazi wote kwa jitihada zao na kujitoa katika kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

..........................................
Prof. Mark J. Mwandosya
**Mwenyekiti wa Bodi**

# DIBAJI

Muhtasari huu wa Taarifa ya Utendaji kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mamlaka za Maji) kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 inatoa uchambuzi wa ulinganisho wa utendaji wa mamlaka za maji dhidi ya malengo yaliyoainishwa katika mipango yao ya biashara, viwango vya huduma, na vigezo vya sekta. Taarifa inatoa muhtasari wa hali ya huduma za maji na usafi wa mazingira, inabainisha changamoto, na inapendekeza hatua za kuchukuliwa ili utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira nchini kuwa za uhakika, salama na kwa gharama stahiki.

Kipindi hiki kimekuwa na maendeleo katika sekta ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/23 hususan katika uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji kwa asilimia 7, maunganisho ya majisafi kwa asilimia 9 na ukusanyaji wa mapato kwa asilimia 7. Aidha kulikuwa na upanuzi wa huduma ambapo idadi ya watu wanaopata maji safi iliongezeka kwa asilimia 3. Ufanisi mwingine uliopatikana ni pamoja na kuimarika kwa uwiano wa maunganisho yaliyofungwa dira za maji kwa asilimia 2.

Hata hivyo, wakati tunatambua mafanikio haya, changamoto bado zipo. Sekta iliendelea kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa maji usiokidhi mahitaji, kiwango kikubwa cha upotevu wa maji, kupungua kwa saa za huduma, utoaji wa huduma za usafi wa mazingira usiotosheleza, upungufu wa miundombinu ya kutibu majisafi na majitaka, na kupungua kwa uwezo wa mamlaka za maji kujiendesha kutokana na mapato yao. Katika kukabiliana na changamoto hizi, juhudi za pamoja za wadau wa sekta ya maji ni muhimu ili kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote waliotoa maoni katika kusukuma mbele dhamira yetu ya kudhibiti huduma za nishati na maji kwa uwazi, ufanisi, na tija ili kuhakikisha ubora, upatikanaji, na unafuu wa huduma hizo. Kwa pamoja, tunaweza kuhakikisha upatikanaji wa huduma za maji safi na usafi wa mazingira, na hivyo kuboresha maisha na maendeleo endelevu ya jamii zetu.

.......................................
Dkt. James A. Mwainyekule
**Mkurugenzi Mkuu**

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| BOD | Mahitaji ya Oksijeni Kibaiolojia (*Biological Oxygen Demand*) |
| CCC | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (*Consumer Consultative Council*) |
| COD | Mahitaji ya Oksijeni Kikemikali (*Chemical Oxygen Demand*) |
| DAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (*Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority*) |
| *E. coli* | Kiashiria cha uchafuzi wa majisafi unaotokana na vimelea *(Escherichia coli)* |
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (*Energy and Water Utilities Regulatory Authority*) |
| HTM | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Handeni Trunk Main |
| IWA | Jumuiya ya Kimataifa ya Wataalam wa Maji *(International Water Association)* |
| KASHWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama-Shinyanga |
| MajIS | Mfumo wa Uwasilishaji Taarifa za Maji Kielektroniki |
| Mamlaka ya Maji | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira |
| MANAWASA | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea |
| RUWASA | Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (*Rural Water Supply and Sanitation Agency*) |

## VIPIMO NA ALAMA


| | |
|---|---|
| % | Asilimia |


# FASILI YA VIASHIRIA VIKUU VYA UTENDAJI


| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| 1 | Muda wa Ukusanyaji wa madeni | Wastani wa muda katika miezi ambayo wateja huchukua kulipa ankara. Inakokotolewa kwa kuchukua jumla ya madeni ambayo mamlaka ya maji inawadai wateja kutokana na huduma ya majisafi na majitaka kwa mwaka ikigawanywa kwa jumla ya mauzo ya maji na majitaka (ankara) ikizidishwa na miezi 12. Utendaji mzuri ni usiozidi miezi miwili (2) | Miezi |
| 2 | Wastani wa saa za huduma | Saa kwa siku ambazo mtumiaji anaweza kupata maji kwenye bomba lililounganishwa moja kwa moja kwenye mtandao wa mamlaka ya maji. Kiwango bora cha huduma ni saa 24 | Saa |
| 3 | Uwiano wa maunganisho ya maji yenye dira | Ni asilimia ya maunganisho ya maji yenye dira za maji zinazofanyakazi. Kiwango kinachotakiwa ni asilimia 100 | (%) |
| 4 | Upotevu wa maji | Tofauti ya kiasi cha maji kinachozalishwa au kinachonunuliwa kutoka mamlaka ya maji nyingine na kilichouzwa. Kiwango kinachokubalika cha upotevu wa maji ni chini ya asilimia 20 | (%) |
| 5 | Uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato | Uwiano wa gharama za uendeshaji kwa mapato. Gharama za uendeshaji inajumuisha gharama zote za uendeshaji pamoja na uchakavu wa miundombinu pamoja na riba. Usimamizi mzuri wa fedha ni ule wenye uwiano wa chini ya 0.8 | Uwiano |
| 6 | Uwiano wa gharama za watumishi kwa kila mita ya ujazo wa maji yanayozalishwa | Uwiano wa jumla ya gharama za watumishi kwa mita za ujazo wa maji yaliyozalishwa kwa mwaka. | Shilingi/mita za ujazo |
| 7 | Uwiano wa idadi ya watu waliopo kwenye eneo lenye mtandao wa maji | Uwiano wa idadi ya watu waliopo ndani ya mita 200 kutoka kwenye bomba la kusambaza maji dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma | Asilimia |

| NA. | KIASHIRIA | TAFSIRI | KIPIMO |
|---|---|---|---|
| 8 | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kwenye maunganisho ya majumbani, kwenye magati/vilula na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma. | Asilimia |
| 9 | Ufanisi wa kukusanya mapato | Uwiano wa jumla ya makusanyo kwa jumla ya ankara. Uwiano huu hukokotolewa kwa kugawanya kiasi cha mapato yaliyokusanywa kwa kiasi cha ankara kilichotozwa kikizidishwa kwa 100 | Asilimia |
| 10 | Tija ya watumishi | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 ya majisafi na majitaka. Inakokotolewa kwa kugawanya jumla ya watumishi kwa jumla ya maunganisho ya majisafi na majitaka ikizidishwa na 1,000. Kiwango kinachofaa ni chini ya watumishi watano kwa kila maunganisho 1,000 | Idadi ya watumishi kwa kila maunganisho 1,000 |
| 11 | Kukidhi viwango vya ubora wa maji | Uwiano wa sampuli za maji zilizopimwa na kukidhi viwango vya ubora. Hupatikana kwa kugawanya idadi ya sampuli zilizokidhi viwango kwa idadi ya sampuli zilizopimwa na kuzidisha kwa 100. Kiwango kinachofaa ni angalau asilimia 98 | Asilimia |
| 12 | Uwiano wa uendeshaji dhidi ya mapato | Uwiano wa gharama za uendeshaji kwa mapato. Usimamizi mzuri wa fedha ni ule wenye uwiano wa chini ya 0.67 | Uwiano |
| 13 | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka | Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya majitaka kwenye maunganisho ya majumbani na kwenye taasisi za bweni dhidi ya idadi ya watu waliopo katika eneo la huduma | Asilimia |
| 14 | Kukidhi viwango vya ubora wa majitaka | Asilimia ya sampuli za majitaka zilizofikia vipimo vya ubora kulingana na viwango vya ubora vya majitaka vilivyowekwa na shirika la viwango (TBS). Asilimia inayokubalika ni angalau 95 | Asilimia |

# UTENDAJIKAZI WA MAMLAKA ZA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

























# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliundwa mwaka 2001 kwa Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na kuanza kazi Septemba 2006. EWURA imepewa mamlaka na sheria hiyo kusimamia shughuli zote za kiuchumi na kiufundi katika sekta za nishati (umeme, petroli na gesi asilia); na maji (majisafi na usafi wa mazingira). Aidha, kifungu cha 7 cha Sheria hiyo, kimeipa EWURA majukumu yafuatayo:

a) kutekeleza kazi zote zilizoainishwa kwenye Sheria ya EWURA na Sheria za Kisekta;
b) kutoa, kuhuisha na kufuta leseni;
c) kuweka na kusimamia viwango vya ubora wa huduma;
d) kudurusu na kusimamia bei za huduma;
e) kutunga sheria ndogo na kanuni;
f) kufuatilia maendeleo ya sekta zinazodhibitiwa kwa kuzingatia upatikanaji, ubora wa huduma, gharama ya huduma, ufanisi wa uzalishaji, uwekezaji na usambazaji wa huduma;
g) kusimamia utatuzi wa malalamiko na migogoro;
h) kutoa taarifa kuhusu kazi za udhibiti;
i) kupata maoni ya mamlaka zingine za kiudhibiti; na
j) kusimamia utekelezaji wa sheria ya 414 iliyoanzisha EWURA.

Kitabu hiki kinatoa muhtasari wa namna EWURA ilivyotimiza jukumu lake la kuisimamia sekta ya maji na matokeo ya tathmini ya utendaji wa mamlaka za maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Taarifa imegawanyika katika sura tano ambazo ni:

Sura ya kwanza inatoa utangulizi wa majukumu ya EWURA yakiwemo ya usimamizi wa sekta ya maji, dira na dhamira ya EWURA, lengo la taarifa, mgawanyo wa mamlaka za maji na nyenzo zilizotumika katika uandaaji wa taarifa;

Sura ya pili inaeleza kuhusu matokeo ya uchambuzi wa utendaji wa mamlaka za maji kwa kuzingatia miongozo mbalimbali;

Sura ya tatu inahusu ushindanishaji wa utendaji wa mamlaka za maji ambayo imeainisha taratibu zilizotumika na matokeo ya ushindanishaji huo;

Sura ya nne ni masuala yaliyobainika na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kupata ufumbuzi na kuongeza ufanisi katika utendaji wa mamlaka za maji nchini; na

Sura ya tano na ya mwisho ni hitimisho la taarifa.

## 1.1 Majukumu ya EWURA katika Sekta ya Maji

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272, [Sheria ya Maji], EWURA imepewa jukumu la kudhibiti huduma zinazotolewa na Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira nchini. Majukumu hayo ni pamoja na:

a) Kutoa leseni kwa watoa huduma za maji na usafi wa mazingira na kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hizo;
b) kutoa miongozo na kanuni mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira;
c) kuchambua na kuidhinisha bei za huduma za maji na usafi wa mazingira;
d) kufuatilia ubora wa maji;
e) kukusanya na kuchambua taarifa za utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira;
f) kufanya stadi mbalimbali kwa ajili ya masuala ya kiutawala na kiuendeshaji katika sekta ya maji; na
g) kuandaa taarifa ya mwaka ya utendaji wa mamlaka za maji na usafi wa mazingira.

Ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika sheria zote mbili, na kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 29 (2) cha Sheria ya Maji, EWURA imeandaa Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 yenye kulinganisha utendaji wa mamlaka za maji 82 kulingana na vigezo vya utendaji vilivyoainishwa kwenye leseni zao. Mamlaka hizo zinajumuisha 25 za mikoa, 7 miradi ya kitaifa, 45 za wilaya na 5 za miji midogo.

## 1.2 Dira na Dhamira ya EWURA

**Dira**
Kuwa mdhibiti wa kiwango cha kimataifa kwa huduma endelevu za nishati na maji.

**Dhamira**
Kudhibiti huduma za nishati na maji kwa uwazi, ufanisi na tija ili kuhakikisha ubora, upatikanaji na unafuu wa huduma hizo.

## 1.3 Lengo la Taarifa

Taarifa ya utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, inalenga kufanya yafuatayo: -

i) Kutoa tathmini ya kina kuhusu hali ya utendaji wa mamlaka za maji nchini katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira;

ii) Kutoa mapendekezo ya kuboresha utoaji wa huduma hizo kutokana na changamoto zilizobainishwa; na

iii) Kuchochea uwajibikaji wa mamlaka za maji katika kuhudumia wananchi.

Katika kutekeleza lengo hili la tathmini, EWURA ilizingatia Mwongozo wa Vigezo vya Utendaji wa EWURA kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022 ambapo tathmini imefanyika kwa kuangalia utendaji wa jumla (overall ranking) katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira wa mamlaka za maji na utendaji kwa kuzingatia utekelezaji wa malengo ya mamlaka hizo katika mipango yao ya biashara (utility ranking).

## 1.4 Mchanganuo wa Mamlaka za Maji

Kifungu cha 14 cha Sheria ya Maji, kinazitaka mamlaka za maji kutekeleza majukumu kwa kuzingatia leseni zinazotolewa na EWURA. Leseni hizo zipo katika madaraja matatu ambayo ni Daraja la I, Daraja la II na Daraja la III. Mamlaka za maji ambazo hazikidhi vigezo vya kupata madaraja hayo ya leseni hupatiwa leseni za muda.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji za Tanga na Moshi ziliendelea kutoa huduma kwa kutumia leseni za Daraja la I, wakati mamlaka za maji za Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, KASHWASA, Babati, Kahama na Iringa ziliendelea na Leseni za Daraja la II. Kwa upande wa Leseni za Daraja la III, mamlaka za maji 61 zilikuwa zikifanya kazi chini ya daraja hili, huku mamlaka za maji 11, ambazo ni Songe, Busega, Kibondo, Itumba-Isongole, Tukuyu, Chunya, Namtumbo, Rujewa, Tunduma, Namanyere, na Tunduru zikifanya kazi chini ya Leseni ya Muda.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 5 (1) ya Kanuni za Sheria ya Maji, mamlaka za maji zimepangwa katika madaraja manne, ambayo ni AA, A, B na C kulingana na uwezo wao wa kifedha na utoaji wa huduma za majisafi.

Aidha, Mwongozo wa Vigezo vya Utendaji wa EWURA kwa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022 pia umeainisha makundi matatu ya mamlaka za maji kulingana na idadi ya wateja ambayo EWURA imetumia kufanya ushindanishaji. Makundi hayo ni pamoja na Kundi la I ni mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000, Kundi la II ni mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na Kundi la III ni mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000.

Kwa ujumla mamlaka za maji zilizojadiliwa katika taarifa hii na madaraja yake, madaraja ya leseni ya usambazaji majisafi na usafi wa mazingira na kundi lake kulingana na uwezo wake wa kutoa huduma yameoneshwa kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa Mamlaka za Maji kwa kuzingatia Leseni, Madaraja na Kundi la Mamlaka**

| Madaraja ya Leseni | | | Madaraja ya Mamlaka | | | Kundi la Mamlaka | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Daraja la Leseni** | **Idadi ya Mamlaka** | | **Daraja** | **Idadi ya Mamlaka** | | **Kundi** | **Idadi ya Mamlaka** |
| I | 2 | | AA | 6 | | Kundi la I (wateja zaidi ya 20,000) | 20 |
| II | 8 | | A | 13 | | Kundi la II (wateja kati ya 5,000 - 20,000 | 22 |
| III | 61 | | B | 10 | | Kundi la III (wateja chini ya 5,000) | 40 |
| Ya Muda | 11 | | C | 53 | | | |

**Fasili ya Madaraja ya Leseni**

| | |
|---|---|
| **Daraja la I** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na mwenye uwezo wa kurejesha gharama zote za uendeshaji |
| **Daraja la II** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma mwenye uwezo wa kiufundi, kiuendeshaji na mwenye uwezo wa kurejesha gharama za uendeshaji isipokuwa sehemu ya gharama za uwekezaji |
| **Daraja la III** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye bado anasaidiwa na Serikali kifedha, kiuendeshaji na kiufundi na ana uwezo wa kurejesha kiasi cha gharama zake za uendeshaji |
| **Leseni ya Muda** | Leseni inayotolewa na EWURA kwa mtoa huduma ambaye hajakidhi vigezo vya kupata leseni ya Daraja la I, II au III (mwenye miundombinu na rasilimali watu kwa ajili ya utoaji wa huduma) |

**Fasili ya Madaraja ya Mamlaka za Maji**

| | |
|---|---|
| **AA** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 85 ya wakazi wake na zinamudu gharama za uendeshaji, matengenezo, uchakavu, na zinaweza kurudisha gharama za uwekezaji |
| **A** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 75 ya wakazi wake na zinamudu gharama zote za uendeshaji, matengenezo na uchakavu |
| **B** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji kwa zaidi ya asilimia 65 na zinamudu gharama zote za uendeshaji na matengenezo |
| **C** | Mamlaka za maji zinazotoa huduma ya maji chini ya asilimia 65 na zinamudu gharama za uendeshaji na matengenezo isipokuwa sehemu ya gharama za umeme wa kuendesha mitambo inagharamiwa na Serikali |

## 1.5 Nyenzo za Uandaaji wa Taarifa

Nyenzo mbalimbali ikiwemo ukusanyaji, uchambuzi na uhakiki wa taarifa za kiufundi, kibiashara na kifedha kutoka mamlaka za maji zilitumika kuandaa taarifa hii. Taarifa na takwimu hizo zilipatikana kupitia mfumo wa kielektroniki wa uwasilishaji taarifa (MajIS), mipango ya biashara, taarifa za fedha na taarifa za utendaji za mwaka.


Njia mbalimbali zilitumika kuhakiki taarifa na takwimu hizo, ikiwemo kufanya ukaguzi kwenye mamlaka za maji, kuomba ufafanuzi pale ambapo takwimu zilionesha mwenendo usio wa kawaida ikilinganishwa na taarifa za awali au ambapo takwimu au maelezo yalikuwa yanakinzana au yasiyo sahihi. Aidha, EWURA ilifanya mikutano na watendaji wakuu wa mamlaka za maji ili kujadili na kuthibitisha taarifa na takwimu zilizopokelewa kabla ya kuchapishwa, mikutano hiyo pia ilihudhuriwa na watendaji kutoka Wizara ya Maji na Wizara ya Afya. Vilevile, EWURA ilifanya mikutano ya mashauriano na Wizara ya Maji na Wizara ya Afya ili kujadili rasimu ya taarifa kabla ya kuchapishwa.

# SURA YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI WA UTENDAJI

Uchambuzi wa kiufundi, kifedha na utendaji wa mamlaka za maji kwa mwaka wa fedha 2023/24 umefanyika kwa kulinganisha utendaji uliofikiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22 na kuonesha matokeo yafuatayo:

### 2.1 Uzalishaji na Mahitaji ya Maji




Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mahitaji ya maji yaliongezeka kwa asilimia 4.6, uzalishaji wa maji kwa asilimia 0.7 na uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji kwa asilimia 7 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/23. Pamoja na ongezeko hilo, uzalishaji wa maji kwa ujumla ulikuwa ni asilimia 45 tu ya mahitaji ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji. Ongezeko hilo la mahitaji ya maji katika maeneo yanayohudumiwa na mamlaka za maji linahusishwa na ongezeko la watu kufuatia ongezeko la maeneo ya huduma ya mamlaka za maji na ongezeko la kawaida la idadi ya watu.

Ukilinganisha na miaka ya nyuma, uwiano wa uzalishaji dhidi ya mahitaji ya maji ulipungua hadi asilimia 45 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 kutoka asilimia 47 katika mwaka wa fedha 2022/23 na asilimia 48 katika Mwaka wa Fedha 2021/22. Kupungua kwa uwiano huu kunamaanisha kuwa, ongezeko la uzalishaji maji halikuendana na kasi ya ongezeko la mahitaji ya maji.


Vilevile, uwiano wa uzalishaji maji dhidi ya uwezo wa mitambo ya uzalishaji maji ulipungua kufikia asilimia 53 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 kutoka asilimia 56 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Kupungua kwa uwiano huu inamaanisha kutotumika ipasavyo kwa miundombinu ya uzalishaji maji iliyopo katika kuboresha upatikanaji wa huduma za maji.

Katika kipindi hicho, uwiano wa mahitaji ya maji dhidi ya uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji ulikuwa ni asilimia 86. Hii ina maanisha kuwa, uwezo wa miundombinu ya uzalishaji wa maji iliyopo haikidhi ongezeko la mahitaji ya maji, hivyo uwekezaji katika miundombinu ya uzalishaji wa maji ni muhimu.

## 2.2 Kiwango cha Upatikanaji wa Maji

### a. Upatikanaji wa huduma ya maji

Uwiano wa idadi ya watu wanaoishi kwenye maeneo yenye mtandao wa maji uliongezeka na kufikia asilimia 84 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 82 na 83 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia. Kuimarika kwa uwiano huu kunatokana na utekelezaji wa miradi ya kuongeza mtandao wa usambazaji maji.




Kwa upande mwingine, uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji uliongezeka hadi asilimia 66 ikilinganishwa na asilimia 63 katika Mwaka wa Fedha 2022/23.


Uchambuzi wa uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji unaonesha kuwa:

i. Mamlaka za maji za Kigoma na Iringa zilifikia zaidi ya asilimia 90 ya huduma ya mtandao wa maji; na

ii. Uwiano wa idadi ya watu wanaopata huduma ya maji kwa mamlaka za maji za Chunya, Itumba-Isongole na Kiomboi ulipungua kwa zaidi ya asilimia 10 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/23 kutokana na ongezeko la maeneo ya huduma ili kufikia maeneo yenye mtandao mdogo wa maji.

### b. Muda wa Upatikanaji wa Huduma ya Maji

Kwa miaka mitatu mfululizo, wastani wa muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ya huduma ya mamlaka za maji kwa siku umeendelea kuwa saa 14. Wastani huo ni chini ya kiwango kinachotakiwa cha saa 24.




Katika mwaka wa fedha wa 2023/24, mamlaka za maji za Moshi, Kahama, KASHWASA, Igunga, Turiani, Makete, Nzega na Orkesumet zilikuwa na muda wa upatikanaji

wa huduma ya maji kwa maeneo ya huduma kwa wastani wa saa 24. Mamlaka za maji za Kahama, KASHWASA, Igunga, Turiani, Makete, Nzega na Orkesumet ziliendelea kutoa huduma ya maji kwa wastani wa saa 24 kama ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Aidha, mamlaka za maji 6 ambazo ni Kondoa, Liwale, Songe, Rombo, Ruangwa na Kibaya zilikuwa na wastani wa muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo yao usiozidi saa tano kwa siku.


## 2.3 Kiwango cha Ubora wa Maji

### a. Miundombinu ya Kusafisha na Kutibu Maji




Katika kipindi cha mapitio asilimia 97.6 ya mamlaka za maji zilikuwa na miundombinu ya kutibu maji ikilinganishwa na asilimia 94 na 91 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia. Aidha, mamlaka za maji 34 kati ya 82 zilitibu maji kwa kutumia mitambo, 46 kwa kutumia dawa mbalimbali za kuua vimelea vya magonjwa kwenye maji kama vile *calcium hypochlorite*. Hata hivyo, mamlaka za maji mbili ambazo ni Songe na Tunduru hazikuwa na miundombinu ya kutibu maji, ikilinganishwa na mamlaka za maji tano na nane katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia.

### b. Ubora wa Maji





Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, kiwango cha ubora wa maji yanayosambazwa na mamlaka za maji kwa kuzingatia viashiria vya vimelea vya magonjwa (*E. coli)* na kiwango cha dawa (residual chlorine) viliimarika wakati kiwango cha tope (*turbidity*) na kiwango cha asidi (pH) vilishuka ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/23.

Kwa ujumla, kiwango cha viashiria vya vimelea vya magonjwa (E. coli) na kiwango cha dawa (residual chlorine) vimeimarika kwa asilimia 4 na 2, mtawalia katika Mwaka wa Fedha 2023/24. Hata hivyo, kiwango cha tope (turbidity) na

asidi (pH) vimeshuka kwa asilimia 14 na 6, mtawalia ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/23. Kutokidhi kiwango cha dawa kunachangiwa na miundombinu ya kutibu maji isiyotosheleza pamoja na kutofuata taratibu katika mchakato wa kutibu maji.

## 2.4 Upatikanaji wa Huduma za Usafi wa Mazingira

### a. Huduma za Majitaka kwa Njia ya Mtandao




Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, idadi ya wateja wanaopata huduma ya majitaka kupitia mtandao wa bomba iliongezeka na kufikia 59,691 kutoka wateja 56,899 na 55,996 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia. Mamlaka za maji za Dodoma, Arusha na Mwanza zilikuwa na ongezeko kubwa zaidi la maunganisho ya mtandao wa majitaka kwa 589, 578 na 417, mtawalia. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na uhamasishaji wa jamii zilizo karibu na mtandao wa majitaka kuunganishwa na mitandao hiyo.

Uchambuzi unaonesha kuwa, uwiano wa idadi ya watu wanaoishi katika eneo lenye mtandao wa majitaka kati ya mamlaka za maji 11 zinazotoa huduma umepungua kufikia asilimia 5.6 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 10.7 na asilimia 13.1 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia. Sababu ya kupungua ni ongezeko la watu katika eneo la huduma la mamlaka za maji ambalo halikuendana na ongezeko la mtandao wa majitaka.

## 2.5 Kiwango cha Ubora wa Majitaka

### a. Miundombinu ya Kutibu Majitaka na Topekinyesi


Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, uwezo wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi katika mamlaka za maji umefikia mita za ujazo 179,305 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 179,295 kwa siku zilizoripotiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Ongezeko hili linatokana na ongezeko la mamlaka za maji zenye miundombinu hiyo kufikia 23 kutoka 21 za Mwaka wa Fedha 2022/23. Mamlaka za maji ambazo miundombinu yake imekamilika na kuanza kufanya kazi ni HTM na Tunduma.

Kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi, mamlaka za maji 10 ambazo ni DAWASA, Tanga, Babati, Bunda, Chato, Musoma,

Igunga, Njombe, Singida na Tabora ziliendelea na ujenzi huo. Mamlaka za maji nyingine sita ambazo ni Namanyere, Ludewa, Kondoa, Mafinga, Makete na Manyoni zimeshapata maeneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka na topekinyesi.


Mamlaka za maji 45 hazikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi wala eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Mamlaka hizo ni Bariadi, Vwawa-Mlowo, KASHWASA, Makonde, MANAWASA, Mpanda, Mpwapwa, Gairo, Mbinga, Ifakara, Utete, Rombo, Itumba-Isongole, Maswa, Mugango-Kiabakari, Wanging'ombe, Biharamulo, Chunya, Karatu, Kasulu, Kibaya, Kibondo, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Kiomboi, Kishapu, Kyela-Kasumulu, Liwale, Loliondo, Lushoto, Mbulu, Mwanhuzi, Namtumbo, Ngara, Orkesumet, Ruangwa, Rujewa, Same-Mwanga, Songe, Tukuyu, Tunduru, Ushirombo, Maganzo, Makambako na Turiani.

### b. Ubora wa Majitaka




Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, kiwango cha ubora wa majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira (effluent) kwa viashiria vya mahitaji ya oksijeni kibiolojia (BOD) na kikemikali (COD) kimeshuka kwa asilimia 25 na 17 ,mtawalia ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2022/23. Sababu kuu ya kushuka kwa viwango vya viashiria hivi ni kutokana na matengenezo duni ya mtandao wa maji taka na mitambo ya kutibu maji taka pamoja na kuzidiwa kwa uwezo wa mitambo hiyo.

## 2.6 Upotevu wa Maji




Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, kiwango cha upotevu wa maji kimeshuka na kufikia asilimia 36.8 ikilinganishwa na asilimia 37.2 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Kiwango hiki cha upotevu wa maji ni sawa na upotevu wa mapato yenye thamani ya shilingi bilioni 114.12 katika kiwango cha huduma kinachokubalika cha asilimia 20.

Katika mwaka wa mapitio, mamlaka za maji 10, ambazo ni Maganzo, Nzega, KASHWASA, Biharamulo, Mwanhuzi, Busega, Gairo, Kishapu, Shinyanga, na Kahama zilikuwa na upotevu wa maji usiozidi asilimia 20.

Uchambuzi unaonesha kuwa, ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/23, katika Mwaka wa Fedha 2023/24 mamlaka za maji nane ziliimarika kwa kupunguza upotevu wa maji kwa zaidi ya asilimia 10. Mamlaka hizo ni Kiomboi (32), Mugango-Kiabakari (27), Wanging'ombe (22), Itumba-Isongole (17), Ifakara (12) Biharamulo (12), Dodoma (11) na Mpanda (11).

## 2.7 Udhibiti wa Upotevu wa Maji

Upotevu wa maji umeendelea kuwa changamoto kwa mamlaka za maji nchini. Katika kukabiliana na changamoto hii, EWURA iliandaa miongozo mbalimbali ukiwemo, Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021. Mwongozo huu unazitaka mamlaka za maji kuhakikisha upotevu wa maji hauzidi asilimia 20 ya maji yanayozalishwa. Aidha, upo Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima na Kufanyia Matengenezo Dira za Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021, unazitaka mamlaka za maji kuwa na sera ya dira za maji na kanzidata. Ili kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa upotevu wa maji na kufikia lengo la kupunguza upotevu huu, uchambuzi umefanyika katika viashiria vifuatavyo:

### a. Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji

Mamlaka za maji na usafi wa mazingira zinatakiwa kuandaa na kutekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji. Mwongozo wa EWURA wa Kupunguza Upotevu wa Maji wa Mwaka 2021 unasisitiza pia juu ya kuandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji kwa mujibu wa mwongozo wa Jumuiya ya Kimataifa ya MajI (IWA) ili kujua maeneo ya upotevu wa maji kwenye mamlaka hizo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji 25 kati ya 82 zilikuwa na mikakati iliyoidhinishwa ya kupunguza upotevu wa maji ikilinganishwa na mamlaka za maji 17 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Mamlaka hizo ni Gairo, Iringa, Dodoma, DAWASA, Utete, Makonde, Bariadi, Biharamulo, Bukoba, Bunda, Busega, Maswa, Musoma, Ngara, Babati, Tanga, Arusha, Moshi, Igunga, Kahama, Nzega, Shinyanga, KASHWASA, Karatu, na Orkesumet. Aidha, mamlaka zote za maji 82 ziliandaa mizania ya kupima viwango vya upotevu wa maji.

### b. Sera ya Dira za Maji

Sera ya Dira ya Maji inalenga kuweka mfumo wa usimamizi wa dira za maji katika maeneo ya huduma ya mamlaka za maji. Pamoja na mambo mengine, sera inalenga pia kuweka utaratibu wa ufungaji wa dira za maji kwa wateja ili kudhibiti upotevu wa maji. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji 31 kati ya 82 zilikuwa na sera za dira za maji zilizoidhinishwa kwa ajili ya

usimamizi wa dira za maji ikilinganishwa na mamlaka za maji 18 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Mamlaka hizo ni Iringa, Manyoni, Mpwapwa, Dodoma, DAWASA, Makonde, Utete, Ruangwa, Bariadi, Biharamulo, Bukoba, Bunda, Busega, Musoma, Mwanza, Ngara, Geita, Tanga, Moshi, Babati, Maswa, Igunga, Kahama, KASHWASA, Kigoma, Nzega, Shinyanga, Arusha, Karatu, Orkesmet na Tabora.

### c. Kanzidata ya Dira za Maji

Mwongozo wa Kuchagua, Kufunga, Kupima na kufanyia matengenezo dira za maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021 unazitaka mamlaka za maji kuwa na -Kanzidata ya Dira za Maji. Kanzidata ya Dira za Maji inawezesha mamlaka za maji kufahamu maeneo ambayo dira za maji zimefungwa ili kurahisisha usomaji wa dira hizo pamoja na usimamizi wa dira za maji. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji sita kati ya 82, ambazo ni Iringa, Moshi, Musoma, Songea, Babati na Makonde zilikuwa na kanzidata za dira za maji.

### d. Uwiano wa Maunganisho yenye Dira za Maji

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, uwiano wa maunganisho ya maji yenye dira za maji uliimarika kwa asilimia 2.2 na kufikia asilimia 95 ikilinganishwa na asilimia 92.8 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Pamoja na uimara huu, uwiano wa maunganisho bado uko chini ya kiwango cha huduma kinachokubalika cha asilimia 100.





Mamlaka za maji 60 kati ya 82 zilikuwa na uwiano wa asilimia 100 wa maunganisho kwa wateja yenye dira za maji. Mamlaka za maji za Kilindoni, Lushoto, Makete, Ifakara, Kasulu, Itumba-Isongole, Tukuyu, na Rujewa zilikuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 10 katika uwiano wa maunganisho yenye dira za maji wakati mamlaka ya maji ya Kyela-Kasumulu ilirekodi uwiano mdogo wa asilimia 1 kutokana na changamoto za kifedha.

## 2.8 Utendaji wa Kifedha


### a. Ukusanyaji wa Mapato

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, jumla ya mapato yaliyokusanywa na mamlaka za maji yaliongezeka kwa asilimia 7 ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 2 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Kwa ujumla, ongezeko hilo lilichangiwa na kuongezeka mauzo ya maji yaliyotokana na ongezeko la idadi ya wateja, uzalishaji wa maji, na marekebisho ya bei kwa baadhi ya mamlaka za maji.





### b. Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato

Ufanisi wa mamlaka za maji katika ukusanyaji wa mapato uliimarika na kufikia asilimia 92 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 91 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Hata hivyo, ufanisi wa jumla katika ukusanyaji wa mapato uliendelea kuwa chini kwa asilimia 3 ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 95.





Mamlaka za maji 20 ambazo ni Mwanza, Igunga, Kiomboi, Kondoa, Nzega, Sengerema, Makambako, Tunduma, Chunya, Mwanhuzi, Mpwapwa, Ifakara, Kasulu, Maswa, Manyoni, Singida, Ushirombo, Ngara, Mugango-Kiabakari na Rujewa zilifikia ufanisi wa ukusanyaji wa mapato wa asilimia 100 huku mamlaka ya maji Kilindoni ikiwa na ufanisi wa chini kabisa wa ukusanyaji wa mapato wa asilimia 52. Kwa upande mwingine, mamlaka za maji 45 zilishindwa kufikia kiwango cha ufanisi kinachokubalika cha asilimia 95.

### c. Wastani wa Bei za Maji




Wastani wa bei za maji uliongezeka kwa asilimia 4 kutoka Shilingi 1,382 kwa mita ya ujazo katika Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi shilingi 1,437 kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Kwa ujumla ongezeko hili lilitokana na kuanza kutumika kwa bei mpya za maji zilizoidhinishwa katika kipindi hicho. Wastani wa bei kwa kila mamlaka zilikuwa kati ya shilingi 300 hadi 3,590 kwa mita za ujazo. Utofauti wa bei kwa kila mamlaka ulitokana na tofauti ya mazingira ya uendeshaji. Mamlaka za maji zilizoanza kutumia bei mpya ni Mbeya, Babati, Arusha, Loliondo, Mombo, Sumbawanga, Dodoma, Bariadi, Makonde, Lindi, Mafinga, na Mbulu.

### d. Uwiano wa Mapato na Gharama za Uendeshaji





Wastani wa uwiano wa uendeshaji (working ratio) wa mamlaka za maji ulizorota hadi uwiano wa 1.31 katika Mwaka wa Fedha 2023/24, kutoka uwiano wa 1.1 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23. Aidha, uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu wa miundombinu dhidi ya mapato (operating ratio) ulizorota hadi kufikia uwiano wa 3.0 ikilinganishwa na uwiano wa 1.7 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Ongezeko la uwiano huu linamaanisha kupungua uwezo wa kujiendesha wa mamlaka nyingi za maji kwa mapato yao. Kiwango kinachokubalika cha uwiano wa uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato ni chini ya 0.67 na 0.80, mtawalia.

Mamlaka ya maji Kilindoni ilifikia kiwango kizuri zaidi cha uwiano wa gharama za uendeshaji *(working ratio)* na uwiano wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato *(operating ratio)* cha 0.67, wakati mamlaka ya maji Namanyere ikiwa na uwiano wa 3.4 wa uwiano wa gharama za uendeshaji *(working ratio)* na Vwawa-Mlowo uwiano wa 56.47 wa gharama za uendeshaji na uchakavu dhidi ya mapato *(operating ratio)*.

## 2.9 Uwiano wa Watumishi na Wateja

Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, uwiano wa watumishi kwa idadi ya kila wateja 1,000 wa majisafi na majitaka ulifikia 4.0 ikilinganishwa na 3.8 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 4.2 katika Mwaka wa Fedha 2021/22. Utendaji huu upo ndani ya kiwango kinachokubalika cha chini ya watumishi 5 kwa kila wateja 1,000. Mamlaka za maji 38 zilikidhi kiwango hiki cha uwiano.




## 2.10 Huduma kwa Wateja

Kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji zote 82 zilikua na mikataba ya huduma kwa wateja iliyoidhinishwa na EWURA. Aidha, mamlaka za maji 18 ambazo ni Arusha, Iringa, Moshi, Musoma, Songea, Sumbawanga, Babati, Geita, KASHWASA, Biharamulo, Bunda, Igunga, Kishapu, Ludewa, Mpwapwa, Ngara, Nzega, na Sengerema zilifanya tafiti za hali ya kuridhika kwa wateja na huduma zinazotolewa na mamlaka hizo katika maeneo yao ya huduma.

Kwa upande wa ufuatiliaji wa malalamiko ya wateja, tathmini inaonesha kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji zilipokea jumla ya malalamiko 390,416. Kwa ujumla, mamlaka za maji zilipiga hatua ndogo katika kushughulikia malalamiko ya wateja ambapo asilimia 61 ya malalamiko yote yalitatuliwa katika Mwaka wa Fedha 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 95.4 katika Mwaka wa Fedha 2022/23.

Mchanganuo wa malalamiko hayo ni kama ifuatavyo: huduma duni kwa wateja, na ukataji wa huduma yaliwakilisha asilimia 1. Aidha, asilimia 30 yalihusu masuala ya majitaka, asilimia 29 yalihusu malalamiko mengineyo, asilimia 15 ya malalamiko yalihusu ukosefu wa maji au msukumo mdogo, asilimia 14 yalihusu uvujaji wa maji, asilimia 6 yalihusiana na masuala ya ankara za malipo, asilimia 3 yalihusu usomaji wa mita, asilimia 2 yalihusu ucheleweshaji wa kuunganishiwa maji, na asilimia 1 yalihusu ubora wa maji.

## 2.11 Uwasilishaji wa Mipango na Taarifa

### a. Uwasilishaji wa Mipango ya Biashara na Programu za Ufuatiliaji wa Ubora wa Majisafi na Majitaka

Katika mwaka wa mapitio, Mamlaka za Maji zote 82 zilikuwa na programu ya ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na majitaka ikilinganishwa na Mamlaka za Maji 78 katika Mwaka wa Fedha 2022/23. Aidha, mamlaka za maji 63 kati ya 82 zilikuwa na mipango ya biashara (*approved business plans*). Mamlaka za maji ambazo hazikuwa na mipango ya biashara ni Geita, Mugango-Kiabakari, Chato, Chunya, Ifakara, Kasulu, Kibondo, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Kiomboi, Kyela-Kasumulu, Liwale, Makete, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Ushirombo, Tunduma na Tunduru.

### b. Uwasilishaji wa Taarifa

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, uzingatiaji wa uwasilishaji wa taarifa ulikuwa asilimia 68, 72, 77, na 95 kwa taarifa za kila mwezi zinazowasilishwa kielektroniki (MajIS), taarifa za kiufundi za mwaka, taarifa za kifedha, na taarifa za mwaka za MajIS, mtawalia. Mamlaka za maji za Arusha, Iringa, Moshi, Songea, Tanga, Biharamulo, Igunga, Itumba-Isongole, Mpwapwa, Nzega, na Songe ziliwasilisha taarifa zote kwa wakati.

## 2.12 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Taarifa iliyopita

Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 ilitoa jumla ya mapendekezo 13 yaliyolenga kuboresha utendaji wa mamlaka za maji. Pendekezo moja lilipaswa liwe limetekelezwa ifikapo Juni 2024, mapendekezo saba ifikapo Juni 2025, mapendekezo mawili Juni 2026, na utekelezaji wa mapendekezo mengine matatu ni endelevu. Tathmini ya hali ya utekelezaji inaonesha kuwa mapendekezo yaliyopaswa kukamilika kufikia Juni 2024 yalitekelezwa kwa sehemu.

Mapendekezo yaliyotolewa ni kama ifuatavyo: -

a) Hadi kufikia Juni 2025, mamlaka za maji ziboreshe kiwango cha dawa kwenye maji yanayosambazwa kwa wateja *(residual chlorine)* kwa kuandaa na kuwa na vituo/sehemu za kupima na kufuatilia viwango vya dawa;
b) Mamlaka za maji kutumia kutumia vifaa vya kupima kiwango cha dawa kenye maji vilivyohakikiwa;
c) Mamlaka za maji kuhakikisha kuwa maji yanatibiwa na wataalam wenye sifa husika;
d) Mamlaka za maji zinapaswa kujenga miundombinu ya ziada ya kutibu majitaka au kuongeza uwezo wa miundombinu iliyopo ili kukidhi mahitaji;

e) Mamlaka za maji zinapaswa kuhakikisha miundombinu ya kutibu majitaka inakarabatiwa mara kwa mara ili kuimarisha ufanisi wake;
f) Mamlaka za maji ziandae mipango ya biashara inayojumuisha mikakati ya kufikia asilimia 95 ya utoaji huduma ya maji. Mikakati hiyo ihusishe upatikanaji wa fedha za uwekezaji kupitia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public Private Partnership);
g) Mamlaka za maji zihakikishe zinandaa mikakati ya kupunguza upotevu wa maji kwa kuzingatia Mwongozo wa EWURA wa Kuandaa Mkakati wa Kupunguza Upotevu wa Maji kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2021;
h) Mamlaka za maji kuhakikisha zinatekeleza mikakati ya kupunguza upotevu wa maji katika maeneo yao;
i) Mamlaka za maji zijumuishe kwenye Mipango Biashara yao mikakati ya kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi;
j) Mamlaka za maji zihakikishe zinatumia kikamilifu uwezo wa miundombinu ya uzalishaji maji iliyopo kwa kuongeza mtandao wa usambazaji maji sambamba na kuongeza wateja;
k) Mamlaka za maji zitoe kipaumbele mapitio ya mipango yao ya biashara ili ziweze kufanya marekebisho ya bei kulingana na gharama halisi za utoaji huduma;
l) Mamlaka za maji zibuni na kutekeleza mikakati ya kuboresha huduma ya usafi wa mazingira kwa kutumia njia jumuishi (City Wide Inclusive Sanitation Approach); na
m) Mamlaka za maji zinapaswa kutekeleza Mwongozo wa EWURA wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na Topekinyesi kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2020.

Aidha, ili kuboresha utendaji wa mamlaka za maji, ushauri ufuatao ulitolewa kwa Wizara ya Maji: -

a) Wizara ya Maji izisaidie mamlaka za maji kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi. Wizara ilishauriwa zaidi kushirikisha sekta binafsi (PPP) kama njia mojawapo inayoweza kuangaliwa kama njia mbadala; na
b) Wizara ya Maji inashauriwa izisaidie mamlaka za maji kuwa na wataalam wa kutosha na wenye sifa kulingana na muundo wa mamlaka za maji uliodhinishwa.

## 2.13 Utekelezaji wa Masharti ya Bei za Maji

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji 16 za Mpwapwa, Dodoma, Mafinga, Mtwara, Makonde, Lindi, Bariadi, Moshi, Mbulu, Babati, Arusha, Lushoto, Orkesumet, Songea, Mbeya na Sumbawanga ziliidhinishiwa bei mpya za huduma zilizo ambatana na masharti ya kutekeleza. Kwa ujumla, utekelezaji wa masharti ya bei za maji umeongezeka na kufikia asilimia 61 ikilinganishwa na asilimia 58 iliyofikiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23.

## 2.14 Utekelezaji wa Maagizo ya Ukaguzi

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, wakati wa ukaguzi na ufuatiliaji wa ubora wa majisafi na majitaka katika mamlaka za maji, EWURA ilitoa jumla ya maagizo 1,246 kwa mamlaka hizo kwa ajili ya utekelezaji. Tathmini inaonesha kuwa, utekelezaji wa maagizo hayo umeshuka na kufikia asilimia 71 ikilinganishwa na asilimia 88 Iliyofikiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/23.

## 2.15 Hali ya Taasisi

Tathmini ya hali ya taasisi ilifanyika kwa kuangalia uhai wa Bodi na idadi ya watumishi katika mamlaka za maji. Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, mamlaka za maji 66 kati ya 82 zilikuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mamlaka za maji ambazo hazikuwa na Bodi ya Wakurugenzi ni Ludewa, Maganzo, Mbinga, Songe, Namanyere, Utete, Namtumbo, Tunduru, Kilindoni, Turiani, Gairo, Kiomboi, Loliondo, Kigoma, Kishapu, na Mwanhuzi. Vilevile, jumla ya watumishi wa mamlaka za maji iliongezeka na kufikia watumishi 6,837 ikilinganishwa na watumishi 6,073 katika Mwaka wa Fedha wa 2022/23 na 5,998 katika mwaka wa fedha 2021/22. Idadi ya watumishi wanawake iliongezeka mfululizo na kufikia 2,179 katika Mwaka wa Fedha wa 2023/24 kutoka 1,750 katika Mwaka wa Fedha 2022/23 na 1,700 katika Mwaka wa Fedha 2021/22.

# SURA YA TATU

## 3.0 UPIMAJI WA UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

### 3.1 Taratibu za Upimaji wa Mamlaka za Maji

Mwongozo wa EWURA wa Upimaji wa Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2022, umetoa mwongozo wa namna ya kupima utendaji wa mamlaka za maji. Katika Mwongozo huo, mamlaka za maji zinapimwa kwa kushindanishwa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni mamlaka za maji zenye wateja zaidi ya 20,000. Kundi la pili ni mamlaka za maji zenye wateja kati ya 5,000 na 20,000, na kundi la tatu ni mamlaka za maji zenye wateja chini ya 5,000. Katika makundi hayo, mamlaka za maji zilipimwa katika makundi mawili ambayo ni;

i. Upimaji wa Jumla (Overall Ranking); Ni upimaji unaongalia namna ambavyo mamlaka ya maji imetekeleza viashiria vya kiutendaji, imefikia viwango vya huduma vinavyokubalika na imetekeleza viwango vinavyotakiwa vya kiudhibiti.

ii. Upimaji kuangalia namna ambavyo mamlaka imetekeleza malengo iliyojiwekea katika mpango biashara wake (Utility Ranking).

### 3.2 Matokeo ya Upimaji

Kwa mujibu wa vigezo vya upimaji, matokeo ya utendaji wa jumla wa mamlaka za maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ni kama ifuatavyo:

**Kundi la I**

i. Mamlaka ya Maji Moshi iliibuka mshindi wa jumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 20 za kundi la kwanza ikiwa na alama 87.4, utendaji huu unatafsiriwa kama bora zaidi. Aidha, Mamlaka ya Maji Rombo imekua na utendaji wa chini zaidi katika katika kundi hili kwa kupata alama 41.5 ambayo ni wastani.

ii. Mamlaka ya Maji Moshi iliibuka mamlaka bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati mamlaka ya maji Rombo ikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi.

**Kundi la II**

i. Mamlaka ya Maji Nzega iliibuka mshindi wa jumla katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 22 za kundi la pili ikiwa na alama 83.9 inayotafsiriwa kama vizuri sana,

wakati Mamlaka ya Maji Chato ikiwa na utendaji wa chini zaidi katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa alama 40.3 ambayo ni wastani.

ii. Mamlaka ya Maji Maswa iliibuka mshindi katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea katika mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji Geita, Kasulu na Chato zikiwa na utendaji wa chini zaidi ambao hauridhishi.

**Kundi la III**

i. Mamlaka ya Maji Orkesumet ilikuwa mshindi wa jumla ikiwa na alama 74 katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira kati ya mamlaka 40 za kundi la tatu, inayotafsiriwa kama vizuri sana, wakati Mamlaka ya Maji Tunduru ikiwa na utendaji wa chini zaidi kwa alama 35 katika utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira, ambayo hairidhishi.

ii. Mamlaka ya Maji Orkesumet iliikuwa bora katika utekelezaji wa malengo iliyojiwekea kwenye mpango wake wa biashara wakati mamlaka za maji za Mugango-Kiabakari, Chunya, Ifakara, Kibondo, Kilindoni, Kilwa-Masoko, Kiomboi, Kyela-Kasumulu, Liwale, Makete, Namanyere, Namtumbo, Ruangwa, Tunduru, Ushirombo na Tunduma zikiwa na utendaji wa chini zaidi na usioridhisha.

Kwa ujumla, Mwaka wa Fedha 2023/24 utendaji wa mamlaka za maji uliendelea kuimarika kutokana na ongezeko la idadi ya mamlaka za maji zenye utendaji unaoanzia vizuri hadi bora zaidi na pia kupungua kwa mamlaka za maji zenye utendaji usioridhisha.

Ulinganishi wa utendaji wa mamlaka za maji kutoka Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2023/24 ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 2.
Matokeo ya Ushindanishaji wa Mamlaka za Maji kwa makundi yote matatu yameainishwa katika jedwali Na. 3-5.

**Jedwali Na.2 Ulinganishi wa utendaji wa jumla wa Mamlaka za Maji kutoka Mwaka wa Fedha 2021/22 hadi 2023/24**

| Mwaka wa Fedha | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** |
|---|---|---|---|
| Idadi ya Mamlaka Zilizoshindanishwa | 90 | 85 | 82 |
| Utendaji wa Jumla (kwa asilimia) | | | |
| Bora zaidi | 0 | 0 | 1 |
| Vizuri sana | 17 | 12 | 16 |
| Vizuri | 29 | 27 | 31 |
| Wastani | 27 | 31 | 32 |
| Usioridhisha | 26 | 13 | 2 |

### Jedwali Na 3: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la I

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishi wa Jumla | | | | Ushindanishi kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) |
| 1 | Arusha | 42.3 | 32.5 | 74.8 | B | Vizuri Sana | 9 | 52.7 | D | Wastani | 12 |
| 2 | Dodoma | 42.9 | 32.4 | 75.3 | B | Vizuri Sana | 7 | 44.4 | D | Wastani | 16 |
| 3 | Iringa | 40.8 | 38.5 | 79.2 | B | Vizuri Sana | 3 | 45.3 | D | Wastani | 15 |
| 4 | Mbeya | 48.5 | 26.3 | 74.8 | B | Vizuri Sana | 8 | 71.7 | B | Vizuri Sana | 2 |
| 5 | Morogoro | 37.0 | 22.0 | 59.0 | C | Vizuri | 17 | 57.0 | C | Vizuri | 8 |
| 6 | Moshi | 51.6 | 35.8 | 87.4 | A | Bora Zaidi | 1 | 75.0 | B | Vizuri Sana | 1 |
| 7 | Musoma | 30.4 | 31.6 | 62.0 | C | Vizuri | 16 | 30.6 | E | Usioridhisha | 19 |
| 8 | Mwanza | 43.8 | 27.2 | 71.0 | B | Vizuri Sana | 11 | 63.9 | C | Vizuri | 4 |
| 9 | Shinyanga | 43.0 | 33.0 | 76.0 | B | Vizuri Sana | 5 | 60.4 | C | Vizuri | 6 |
| 10 | Songea | 52.2 | 29.0 | 81.3 | B | Vizuri Sana | 2 | 63.2 | C | Vizuri | 5 |
| 11 | Tabora | 33.1 | 24.0 | 57.1 | C | Vizuri | 18 | 40.0 | D | Wastani | 17 |
| 12 | Tanga | 44.4 | 31.3 | 75.7 | B | Vizuri Sana | 6 | 49.0 | D | Wastani | 14 |
| 13 | Bukoba | 39.8 | 27.8 | 67.7 | C | Vizuri | 13 | 55.9 | C | Vizuri | 9 |
| 14 | Kigoma | 33.9 | 20.4 | 54.3 | D | Wastani | 19 | 38.3 | E | Usioridhisha | 18 |
| 15 | Babati | 41.9 | 34.8 | 76.7 | B | Vizuri Sana | 4 | 67.3 | C | Vizuri | 3 |
| 16 | Kahama | 39.0 | 32.6 | 71.6 | B | Vizuri Sana | 10 | 55.5 | C | Vizuri | 10 |
| 17 | DAWASA | 40.2 | 29.9 | 70.1 | B | Vizuri Sana | 12 | 50.8 | D | Wastani | 13 |
| 18 | KASHWASA | 36.8 | 30.4 | 67.2 | C | Vizuri | 14 | 54.8 | D | Wastani | 11 |
| 19 | Singida | 43.7 | 21.5 | 65.2 | C | Vizuri | 15 | 59.6 | C | Vizuri | 7 |
| 20 | Rombo | 25.2 | 16.4 | 41.5 | D | Wastani | 20 | 28.7 | E | Usioridhisha | 20 |

## Jedwali Na. 4: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la II

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishi wa Jumla | | | | Ushindanishi kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) |
| 1 | Mtwara | 33.9 | 19.3 | 53.2 | D | Wastani | 18 | 52.3 | D | Wastani | 4 |
| 2 | HTM | 24.2 | 18.8 | 43.0 | D | Wastani | 21 | 7.1 | E | Usioridhisha | 19 |
| 3 | Sumbawanga | 37.3 | 24.2 | 61.5 | C | Vizuri | 8 | 23.4 | E | Usioridhisha | 18 |
| 4 | Lindi | 33.1 | 22.0 | 55.1 | C | Vizuri | 13 | 38.9 | E | Usioridhisha | 13 |
| 5 | Geita | 27.4 | 26.2 | 53.6 | D | Wastani | 16 | 0.0 | E | Usioridhisha | 20 |
| 6 | Mpanda | 31.2 | 22.8 | 54.0 | D | Wastani | 14 | 31.1 | E | Usioridhisha | 15 |
| 7 | Njombe | 36.6 | 25.6 | 62.2 | C | Vizuri | 6 | 49.6 | D | Wastani | 6 |
| 8 | MANAWASA | 40.6 | 16.1 | 56.7 | C | Vizuri | 10 | 55.9 | C | Vizuri | 3 |
| 9 | Wanging'ombe | 31.5 | 19.4 | 50.9 | D | Wastani | 19 | 42.0 | D | Wastani | 11 |
| 10 | Bunda | 40.1 | 27.3 | 67.3 | C | Vizuri | 4 | 43.8 | D | Wastani | 10 |
| 11 | Igunga | 44.1 | 36.4 | 80.5 | B | Vizuri Sana | 2 | 49.5 | D | Wastani | 7 |
| 12 | Karatu | 32.6 | 25.2 | 57.8 | C | Vizuri | 9 | 46.9 | D | Wastani | 9 |
| 13 | Maswa | 41.2 | 26.2 | 67.4 | C | Vizuri | 3 | 71.9 | B | Vizuri Sana | 1 |
| 14 | Nzega | 47.5 | 36.4 | 83.9 | B | Vizuri Sana | 1 | 66.1 | C | Vizuri | 2 |
| 15 | Sengerema | 35.4 | 18.6 | 54.0 | D | Wastani | 15 | 39.5 | E | Usioridhisha | 12 |
| 16 | Tukuyu | 31.2 | 22.4 | 53.5 | D | Wastani | 17 | 24.9 | E | Usioridhisha | 16 |
| 17 | Makambako | 40.3 | 22.5 | 62.8 | C | Vizuri | 5 | 50.8 | D | Wastani | 5 |
| 18 | Mbinga | 38.0 | 17.9 | 55.9 | C | Vizuri | 11 | 33.0 | E | Usioridhisha | 14 |
| 19 | Kasulu | 26.6 | 16.8 | 43.4 | D | Wastani | 20 | 0.0 | E | Usioridhisha | 20 |
| 20 | Kondoa | 36.8 | 18.5 | 55.3 | C | Vizuri | 12 | 47.6 | D | Wastani | 8 |
| 21 | Chato | 28.3 | 12.0 | 40.3 | D | Wastani | 22 | 0.0 | E | Usioridhisha | 20 |
| 22 | Busega | 35.3 | 26.4 | 61.7 | C | Vizuri | 7 | 24.2 | E | Usioridhisha | 17 |

**Jedwali Na. 5: Matokeo ya Ushindanishi wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira - Kundi la III**

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishi wa Jumla | | | | Ushindanishi kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) |
| 1 | Bariadi | 33.5 | 25.3 | 58.8 | C | Vizuri | 14 | 16.3 | E | Usioridhisha | 23 |
| 2 | Vwawa-Mlowo | 32.3 | 18.8 | 51.1 | D | Wastani | 23 | 42.7 | D | Wastani | 14 |
| 3 | Makonde | 30.3 | 30.9 | 61.2 | C | Vizuri | 11 | 33.3 | E | Usioridhisha | 18 |
| 4 | Mugango-Kiabakari | 24.9 | 10.6 | 35.5 | E | Usioridhisha | 39 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 5 | Biharamulo | 40.5 | 30.6 | 71.0 | B | Vizuri Sana | 2 | 42.6 | D | Wastani | 15 |
| 6 | Chunya | 35.6 | 13.0 | 48.6 | D | Wastani | 26 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 7 | Gairo | 38.8 | 23.6 | 62.3 | C | Vizuri | 8 | 49.9 | D | Wastani | 10 |
| 8 | Ifakara | 28.8 | 14.2 | 43.0 | D | Wastani | 34 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 9 | Itumba-Isongole | 32.8 | 20.9 | 53.7 | D | Wastani | 20 | 67.5 | C | Vizuri | 3 |
| 10 | Kibaya | 36.1 | 18.8 | 54.9 | D | Wastani | 18 | 54.0 | D | Wastani | 7 |
| 11 | Kibondo | 34.7 | 19.0 | 53.6 | D | Wastani | 21 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 12 | Kilindoni | 25.4 | 16.7 | 42.0 | D | Wastani | 36 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 13 | Kilwa Masoko | 35.4 | 17.6 | 53.0 | D | Wastani | 22 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 14 | Kiomboi | 31.2 | 11.0 | 42.2 | D | Wastani | 35 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 15 | Kishapu | 38.1 | 23.8 | 61.8 | C | Vizuri | 9 | 44.9 | D | Wastani | 12 |
| 16 | Kyela-Kasumulu | 28.5 | 13.1 | 41.6 | D | Wastani | 37 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 17 | Liwale | 26.2 | 15.0 | 41.2 | D | Wastani | 38 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 18 | Loliondo | 43.5 | 23.4 | 66.9 | C | Vizuri | 5 | 57.3 | C | Vizuri | 6 |
| 19 | Ludewa | 35.5 | 25.9 | 61.4 | C | Vizuri | 10 | 67.0 | C | Vizuri | 4 |
| 20 | Lushoto | 42.2 | 21.4 | 63.6 | C | Vizuri | 6 | 64.2 | C | Vizuri | 5 |

| Na | Jina la Mamlaka | Jumla ya Alama kulingana na Vigezo vya Upimaji | Jumla ya Alama kulingana na kukidhi Vigezo vya Kiudhibiti | Ushindanishi wa Jumla | | | | Ushindanishi kwa kufikia Malengo ya Mipango Biashara | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) | Jumla Kuu ya Alama | Daraja | Tafsiri | Nafasi ya Ushindi (2023/24) |
| 21 | Mafinga | 35.9 | 20.0 | 55.8 | C | Vizuri | 17 | 22.1 | E | Usioridhisha | 21 |
| 22 | Makete | 30.3 | 15.6 | 45.8 | D | Wastani | 31 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 23 | Manyoni | 42.3 | 28.0 | 70.3 | B | Vizuri Sana | 3 | 49.0 | D | Wastani | 11 |
| 24 | Mbulu | 36.5 | 21.1 | 57.6 | C | Vizuri | 15 | 44.4 | D | Wastani | 13 |
| 25 | Mpwapwa | 33.9 | 25.9 | 59.7 | C | Vizuri | 12 | 29.8 | E | Usioridhisha | 19 |
| 26 | Mwanhuzi | 34.4 | 14.5 | 48.9 | D | Wastani | 24 | 40.0 | E | Usioridhisha | 16 |
| 27 | Namanyere | 30.0 | 16.1 | 46.1 | D | Wastani | 30 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 28 | Namtumbo | 28.3 | 15.6 | 43.9 | D | Wastani | 33 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 29 | Ngara | 32.7 | 30.5 | 63.2 | C | Vizuri | 7 | 35.4 | E | Usioridhisha | 17 |
| 30 | Orkesumet | 44.5 | 29.4 | 74.0 | B | Vizuri Sana | 1 | 69.5 | C | Vizuri | 1 |
| 31 | Ruangwa | 27.7 | 20.9 | 48.6 | D | Wastani | 25 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 32 | Rujewa | 36.5 | 20.1 | 56.6 | C | Vizuri | 16 | 67.7 | C | Vizuri | 2 |
| 33 | Same-Mwanga | 29.3 | 18.1 | 47.4 | D | Wastani | 28 | 27.1 | E | Usioridhisha | 20 |
| 34 | Songe | 23.7 | 20.8 | 44.5 | D | Wastani | 32 | 18.6 | E | Usioridhisha | 22 |
| 35 | Tunduru | 23.0 | 12.0 | 35.0 | E | Usioridhisha | 40 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 36 | Ushirombo | 34.4 | 12.9 | 47.3 | D | Wastani | 29 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 37 | Utete | 26.8 | 27.8 | 54.6 | D | Wastani | 19 | 11.9 | E | Usioridhisha | 24 |
| 38 | Maganzo | 37.3 | 22.4 | 59.7 | C | Vizuri | 13 | 52.8 | D | Wastani | 9 |
| 39 | Tunduma | 25.9 | 22.0 | 47.9 | D | Wastani | 27 | 0.0 | E | Usioridhisha | 25 |
| 40 | Turiani | 43.1 | 24.4 | 67.5 | C | Vizuri | 4 | 53.5 | D | Wastani | 8 |

# SURA YA NNE

## 4.0 MASUALA YALIYOBAINIKA NA MAPENDEKEZO

Kufuatia tathmini ya Taarifa ya Utendaji wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/24, changamoto mbalimbali zimebainika ambazo EWURA kama mdhibiti inazitolea mapendekezo ili kuweza kufikia malengo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira. Masuala yaliyobainika kutokana na uchambuzi huo na mapendekezo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Masuala yaliyobainika na Mapendekezo**

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kutokidhi kiwango cha ubora wa maji | Wastani wa kukidhi viwango vya ubora wa maji vilikuwa chini ya kiwango cha huduma kinachokubalika katika Mwaka wa Fedha 2023/24 | Mamlaka za maji ziimarishe ubora wa maji kwa:<br>i) kuandaa na kutekeleza Mwongozo wa utaratibu wa kutibu maji *(Standard Operating Procedures)*;<br>ii) Kuwa na vifaa vya kupima kiwango cha dawa, ubora wa maji kwa ajili ya kufuatilia vigezo mbalimbali vya ubora ikiwamo kiwango cha dawa na vimelea vya magonjwa;<br>iii) Kutibu maji kwa kutumia wataalam wenye sifa stahiki. | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Wizara ya Maji iwezeshe mamlaka za maji kujenga miundombinu ya kutibu maji. | Juni 2030 | Wizara ya Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Kutokidhi viwango vya ubora wa majitaka | Wastani wa kiwango cha ubora wa majitaka yaliyotibiwa na kurudishwa kwenye mazingira ulikuwa asilimia 33 ambayo haikidhi viwango vya huduma vinavyotakiwa vya asilimia 100 katika Mwaka wa Fedha 2023/24 | Mamlaka za maji zinaelekezwa:<br>i) Kuongeza uwezo wa miundombinu iliyopo au kujenga miundombinu ya ziada au mipya ili kukidhi mahitaji ya kutibu maji; na<br>ii) kufanya ukarabati wa miundombinu iliyopo mara kwa mara ili kuleta ufanisi | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| 3. | Huduma ya maji isiyotosheleza | Wastani wa mtandao wa maji katika maeneo ya huduma ya mamlaka za maji ulikuwa ni asilimia 84 ambayo ni chini ya asilimia 95 ya lengo la Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 | Mamlaka za maji zinaelekezwa kuweka mikakati ya kufikia asilimia 95 ya mtandao wa maji katika Mipango yao ya Biashara ikiwa ni pamoja na kuingia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| 4. | Utekelezaji hafifu wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja | Kwa wastani ni asilimia 14 tu ya wateja wapya ndiyo waliunganishwa na huduma ya maji ndani ya siku saba za kazi baada ya kukamilisha malipo | Mamlaka za maji zihakikishe wateja wapya wanaunganishiwa huduma ya maji kwa wakati | Endelevu | Mamlaka za Maji |
| 5. | Upotevu wa maji | Wastani wa upotevu wa maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ulikuwa asilimia 36.7, ambayo ni juu ya kiwango kinachokubalika cha asilimia 20 au chini. | Mamlaka za maji ziandae na kutekeleza mkakati wa kupunguza upotevu wa maji | Endelevu | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. | Miundombinu isiyotosheleza kutibu majitaka na topekinyesi | Mamlaka za maji 51 kati ya 82 hazikuwa na miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi hali inayoashiria hatari kwa afya na mazingira. | Mamlaka za maji ziainishe kwenye Mipango ya Biashara mpango mikakati ya kupata eneo la kujenga miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi. | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Wizara ya Maji iziwezeshe mamlaka za maji kupata fedha za ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi. | Juni 2030 | Wizara ya Maji |
| | | | Ushirikishwaji wa sekta binafsi ufanyike kwenye ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka na topekinyesi | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| 7. | Uwiano mdogo wa uzalishaji wa maji ikilinganishwa na mahitaji, na uwezo wa mitambo ya uzalishaji usiotosheleza mahitaji wala kutumika ipasavyo | Wastani wa uwiano wa uzalishaji maji dhidi ya mahitaji ni asilimia 45 na uwiano wa uzalishaji maji dhidi ya uwezo wa miundombinu ni asilimia 54, ikiwa uwiano zinapaswa kuwa asilimia 100 | Mamlaka za maji ziongeze mtandao wa usambazaji maji, uwezo wa miundombinu iliyopo ya uzalishaji na idadi ya wateja ili kukidhi mahitaji | June 2030 | Mamlaka za Maji |

| Na. | Suala Kuu | Yaliyobainika | Mapendekezo | Tarehe ya mwisho ya utekelezaji | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | Bei za maji zilizopitwa na wakati na zisizoendana na gharama halisi za uendeshaji | Baadhi ya mamlaka za maji kuendelea kutumia bei zisizowezesha kurejesha gharama za uendeshaji | Maandalizi ya mipango ya biashara inayoakisi gharama halisi za uendeshaji zitakazojumuishwa kwenye marekebisho ya bei mpya za maji yapewe kipaumbele. | Juni 2026 | Mamlaka za Maji |
| | | | Wizara ya Maji inashauriwa kuziwezesha mamlaka za maji kuwa na wataalam wanaokidhi miundo yao ya utendaji. | Juni 2026 | Wizara ya Maji |
| | | | Wadau muhimu katika mchakato wa marekebisho ya bei za maji wazingatie sheria zilizopo. | Endelevu | Wizara ya Maji |
| 9. | Huduma za usafi wa mazingira zisizotosheleza | Wastani wa mtandao wa majitaka ulikuwa asilimia 5.6 ambao ni chini ya lengo la asilimia 30 lililoainishwa katika wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 | i) Mamlaka za maji zibuni na kutekeleza programu jumuishi za usafi wa mazingira *(Inclusive Sanitation Approach)*;na<br>ii) Mamlaka za maji zitekeleze Mwongozo wa EWURA wa Usimamizi wa Huduma ya Majitaka na topekinyesi kwa Mamlaka za Maji wa Mwaka 2020 | Endelevu | Mamlaka za Maji |

# SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Mafanikio ya utendaji wa mamlaka za maji yaliyopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 ni hatua muhimu, lakini zipo changamoto zilizobainishwa na zinazohitaji jitihada na mipango shirikishi zaidi ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa ya uhakika wa upatikanaji wa huduma bora za majisafi na usafi wa mazingira nchini. Inatarajiwa kwamba, endapo mamlaka za maji zitatekeleza kikamilifu mapendekezo yaliyobainishwa katika taarifa hii, huduma ya majisafi na usafi wa mazingira itaimarika. Aidha, taarifa hii inasisitiza umuhimu wa mamlaka za maji kuongeza juhudi katika kuboresha huduma kwa wananchi.

EWURA itaendelea kuishauri Serikali kuandaa sera, sheria na kanuni zitakazoiwezesha sekta ya maji na usafi wa mazingira nchini kuendelea kukua na kuimarika kwa maendeleo endelevu na manufaa ya taifa letu. Aidha, EWURA itaendelea kuzisimamia Mamlaka za Maji ili ziendeshwe kwa ufanisi zaidi na hatimaye kutoa huduma bora za maji na usafi wa mazingira kwa wananchi.

# MAELEZO:

# MAELEZO:

# MAELEZO:

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001: 2015 Certified


**EWURA Makao Makuu**

**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**

**S.L.P 2857, Dodoma, Tanzania • Simu: +255 26 2329002-4**

**Nukushi:+255 26 2329005 • Tovuti: www.ewura.go.tz**

**Barua Pepe: info@ewura.go.tz**

**Simu ya Bure: 0800110030**

EWURATanzania EWURATanzania EWURATanzania EWURATV